**LEARNING BY EAR**

**“Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii”**

**KIPINDI 9: “Vita dhidi ya mihadarati”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Ludger Schadomsky, Adrian Kriesch**

**PROOFREADER: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: AT THE AIRPORT**

- **Mhe. Kizito (m, 55)**
- **Mugo (m, 40)**
- **3 Journalists (sex and age not important)**

**SCENE TWO: CHUNGA SANA BUS STOP**

- **Chambo (m, 30)**
- **Jabali (m, 18)**
- **Zula (m,18)**
- **Jane (f, 35)**

**SCENE THREE: IN A CAFETERIA**

- **Beri (f, 45)**
- **Waziri Kafegi (m, 55)**

- **Inspekta Tino (m, 40)**
- **Presenter (f, 25)**

## SCENE FOUR: AT HOME WITH ZULA AND CHAMBO

- **Jabali (m, 18)**
- **Mugo (m, 40)**

**MSIMULIZI (mume/mke)**

**INTRO:**

Hamjamboni nyote na karibuni katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki kikiwa ni kipindi cha tisa tukiangazia matumizi ya mihadarati na athari zake. Katika kipindi kilichopita, simanzi ilitanda pale Jabali na Zula walipomkuta Okosho amekata roho baada ya kutumia kiwango kikubwa cha madawa haramu. Kamishna Beri na Inspekta Tino wote walijiuzulu na baadaye, Beri akaenda kumwaga mtama kwa wanahabari kuhusu kesi ya mihadarati iliyohusisha watu wakuu serikalini. Akiwepo Mheshimiwa Kizito, mbunge wa eneo hilo pamoja na Mheshimiwa Kafegi, waziri wa mambo ya ndani. Tuliachia pale Zula na Jabali wakimsubiri Chambo huku wakiulizana mbona kachelewa hivyo. Ni kipi kilichomfikia? Sikiliza. Kipindi cha leo ni **"Vita dhidi ya mihadarati"**, twatandika jamvi pale Mheshimiwa Kizito akiwasili uwanja wa ndege.

## SCENE ONE: AT THE AIRPORT

1. **SFX: AIRPORT ANNOUNCEMENT OF ARRIVALS AND DEPARTURES**

2. **MHE. KIZITO:** Wewe! Unaweza kunipelekea mzigo kwenye gari?

3. **SFX: LUGGAGE ON WHEELS BEING PULLED**

4. **MHE. KIZITO:** Nitakusubiri hapo nje.

5. **SFX: SLIDING DOOR OPENS**

6. **MHE. KIZITO:** **(shocked)** Sasa kunani tena?

7. **SFX: SHOUTS AND SEVERAL CAMERA FLASHES FOR A WHILE**

8. **MUGO:** Mhe. Kizito! Mimi ni Mugo kutoka gazeti la “The Voice”. Je ni kweli kwamba wewe ni mshukiwa mkuu katika kesi inayohusu sheheni kubwa ya heroini iliyopatikana?

9. **MHE. KIZITO:** Kasema nani? Huko ni kuniharibia jina – maadui wangu kisiasa wananipiga vita kwa kila njia.

10. **MUGO:** Kuna thibitisho kuwa mihadarati ilipatikana kwako nyumbani, ikiwa imefichwa ndani ya sehemu za magari unayoagiza kutoka nje.

11. **MHE. KIZITO:** **(trying to act shocked)** Ati!? Lini? Nayasikia leo hayo mimi.

12. **MUGO:** Kwa hivyo unakataa kufanya biashara haramu na Puyanga? Unajuwa tayari yuko kifungoni.

13. **MHE. KIZITO:** Sina la ziada.

14. **SFX: POLICE SIRENS APPROACHING**

15. **MHE. KIZITO:** Hawa ni kina nani? Kwani leo nakaribishwa na msafara wa Rais?

16. **MUGO:** Huu si msafara wa Raisi..Mheshimiwa, nikidhani hao ni askari, kitengo cha kupambana na mihadarati.

17. **MSIMULIZI:** Mugo alisema kweli. Askari wa kikosi cha kupambana na dawa la kulevya lkutokana na shinikizo la polisi wa kimataifa pamoja na taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari walilazimika kuchukua hatua.Na mheshimiwa Kizito ndio walimlenga kwanza. Atakayefuata ni nani? Kwa sasa, katika kituo cha basi, Jabali karibu anapoteza subira ya kumngojea Chambo.

## SCENE TWO: CHUNGA SANA BUS STOP

| | | |
|---|---|---|
| 18. | **SFX: BUSY STREET AMBIENCE** | |
| 19. | **ZULA:** | Jabali, Rafiki yako hatakuja. Twende zetu. |
| 20. | **JABALI:** | Angeliniambia jana. Labda alikuwa na mkutano na waathiriwa wengine. Idadi yao ni kubwa sasa– unajuwa, madawa yanaathiri watu kwa kila njia. |
| 21. | **ZULA:** | Sawa, Twende ili tumwepuke yule mlevi anayekuja hii njia yetu. |
| 22. | **JABALI:** | Mlevi yupi? Yuwapi? |
| 23. | **ZULA:** | Hapo nyuma yako. |
| 24. | **JABALI:** | **( shocked )** Chambo?! Si wewe? Kwani kumetokea nini tena? |
| 25. | **CHAMBO:** | **(drunken stupor)** Ah… ah… Jaba…li… Twende kazini. |
| 26. | **SFX: CHAMBO FALLS DOWN** | |
| 27. | **ZULA:** | Usiniambie yule jamaa ni huyu… Jabali – huyu siye yule aliyekuwa kilabu 2000? |

28. **JABALI:** Ndiye, ni huyu Chambo. Lakini... sijui nikueleze nini. Unafikiri amerudi nyuma?

29. **ZULA:** Kurudi nyuma kivipi!? Huyu hata kusimama wima ni taabu. Wamaanisha nini kurudi nyuma?

30. **JABALI:** Tulipozuru kituo cha kurekebisha tabia, Chambo alinieleza kuwa wale ambao hawakushikilia matibabu kwa makini basi huweza kurudia utumiaji wa madawa hayo au vileo hivyo.

*31.* **ZULA:** **( sings Amy Winehouse song )** ***They tried to make me go to rehab, I said, "No, no, no". He's tried to make me go to rehab, I won't go, go, go***

32. **JABALI:** **(serious)** Hatuna wakati wa mzaha, Zula! Madawa yamemuuwa rafiki yetu Okosho, wewe na Chambo nyote munahitaji msaada… Sijui nitamsaidiaje?

33. **ZULA:** Mpeleke nyumbani, wacha shtimu iishe kwanza. Alafu tuzungumze naye.

34. **JABALI:** **(excited)** Hilo ni wazo zuri! Sasa, nisaidie tumsaidie. Ah! Ni mzito sana.

35. **SFX: JABALI AND ZULA HEAVE CHAMBO UP ONTO THEIR SHOULDERS – GRUNTS AND NOISES OF PHYSICAL EFFORT (studio)**

36. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

37. **JABALI:** Hiyo ni simu yako inaita, Zula?

38. **ZULA:** Wapi, mameni, yangu niliiuza kitambo… nikanunua… si unajuwa tena…

39. **JABALI:** Basi ni simu ya Chambo! Hebu dakika moja.

40. **SFX: FUMBLING IN POCKET (studio)**

41. **JABALI:** **(answers phone)** Halo, Jabali hapa.

42. **JANE:** **(at the phone)** Jabali? Habari… huyu ni Jane. Unanikumbuka? Nimerudi kazini sasa baada ya kuacha uvutaji wa tumbaku. Naweza kuzungumza na Chambo? Nina habari zake njema.

43. **JABALI:** Ah, kweli, Jane! Chambo hawezi kuwasiliana na wewe hivi sasa. Labda nimpe ujumbe wako baadae.

44. **JANE:** Tafadhali mwambie kuwa wakubwa wangu kazini wamefurahia maendeleo yangu na wako tayari kuungana na Chambo ili kuanzisha kampeni ya kupinga mihadarati! Watampa afisi na mshahara na hata wanataka kumpa vifaa vyengine ili kuenuwa kituo hicho cha kurekebisha tabia. Si ni jambo zuri hilo?

45. **JABALI:** **(thrilled)** Siamini! Hilo ni jambo zuri sana!

46. **ZULA:** Jamani nimechoka huyu mlevi yuwalemea...

47. **JANE:** Pole, Sikusikia umesemaje.

48. **JABALI:** Ati? sikuwa mimi… ni rafiki yangu Jane, shukrani kwa simu yako. Nitamuarifu Chambo. Kwaheri.

49. **ZULA:** **(curious)** Mmmh… Jane sio. Inaonekana una mengi yakunieleza.

50. **JABALI:** Sivyo unavyofikiria. Nilimjuwa Jane kupitia Chambo. Lakini Zula, kama ilivyo wewe na Okosho muliwahi kutumia bomba moja, na umenieleza mara nyingi usiku wenu ulikuwa na vituko kila aina … Nafikiri ni muhimu ukapimwe virusi vya ukimwi.

51. **ZULA:** Acha zako! Mambo gani sasa wasema? Kwani mimi naonekana kama mwenye virusi vya ukimwi?

52. **MSIMULIZI:** Jabali hakukosea. Muda mfupi aliokuwa na Chambo alijifunza kuwa mabomba ni njia mojawapo ya kuambukizwa ukimwi hasa yatumiwapo kwa kila mtumizi kujidunga heroini na kokeini. Je, Zula atakubali kupimwa virusi? Na akikubali, majibu yatakuwa nini? Chambo juhudi zake zimeanza kuzaa matunda. Je, Chambo ataepuka mihadarati? Endelea kusikiliza – Hivi punde jibu tutalipata. Si mbali, Beri na Tino walikuwa wanapata vikombe vya chai katika mgahawa fulani wakati Beri akapokea simu.

**SCENE THREE: IN A CAFETERIA**

53. **SFX: CAFE AMBIENCE + RADIO MUSIC**

54. **TINO:** Hivi sasa ambavyo mumewako amefungwa jela, si tuoane, tuishi raha mustarehe ijapokuwa tutakuwa hatuna kitu.

55. **BERI:** **( laughs shyly)** Hauoni haya, Tino.

56. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

57. **TINO:** Yaonekana sio mimi peke yangu ambae nimekumezea mate.

58. **BERI:** Niamini, huyu siye kamwe. Ni simu hata sijui ni ya nani. **(answers call)** Halo, Mhe. Kafegi. Nikusaidie na nini?

59. **MHE. KAFEGI:** Kamishna Beri, kufuatilia rekodi yako nzuri, umepelekwa kitengo cha kitaifa cha askari wa kupambana na mihadarati. Fika kazini haraka iwezakanavyo.

60. **BERI:** **(in total shock)** Eh… eh…

61. **SFX: MOBILE PHONE CALL DISCONNECTED**

62. **TINO:** Kwani .. kuna nini?

63. **SFX: MOBILE RINGING WITH DIFFERENT TONE**

64. **BERI:** Jibu hiyo simu kwanza.

65. **TINO:** **(answers call)** Tino hapa.. Nani mwenzangu?

66. **MHE. KAFEGI:** Inspekta Tino. Umeregeshwa kazini. Utamsaidia kamishna Beri katika kitengo cha kitaifa cha kupambana na mihadarati. Wasili kazini haraka.

67. **TINO:** **(in total shock)** Ah… ah…

68. **SFX: MOBILE PHONE CALL DISCONNECTED**

69. **TINO:** Haya ni kweli?

70. **BERI:** Ikiwa ni kauli ya waziri wa mambo ya ndani nchini, mheshimiwa Kafegi, basi naamini. Ni kweli….

71. **TINO:** Basi tunasubiri nini? Twende kazini!

72. **BERI:** Hebu taratibu kidogo, Inspekta. Umewahi kufikiri kama ni mtego itakuwaje?

73. **TINO:** Mtego? Mtego gani? Hicho ni kitengo kimoja wapo cha askari ambao wana uhuru wa kivyao, kisha hawajalaumiwa na kashfa za ufisadi.

74. **BERI:** Kweli, nafahamu. Lakini waziri haja jitoa kwenye shutma. Labda anajaribu kututumia, anataka kutuingiza kwenye shida hii kwa sababu kabla ya mzigo mkubwa kama ule wa mihadarati uingie nchini ni lazima watu wakubwa serikalini wahusike – watu wenye mamlaka serikalini.

75. **TINO:** Beri, unasema kwe…

76. **SFX: NEWS BEING READ ON THE RADIO.**

77. **BERI:** Muhudumu, hebu tuongezee sauti ya redio yako?

78. **MTANGAZAJI:** Habari zilizotufikia sasa hivi ni kwamba! Aliyekuwa waziri wa mambo ya ndani ya nchi, ajiuzulu. Waziri Kafegi ambae ameshutuhumiwa kuhusika kwa biashara ya mihadarati nchini amejiuzulu ili kuupa uchunguzi nafasi. Mshukiwa mwengine, Puyanga, mfanyi biashara na rafiki mkubwa wa mheshimiwa Kizito,amehukumiwa kifungo cha miaka kumi na tano. Inasemekana kuwa vigogo serikalini pia wanahusika katika sakata hili. Waziri Kafegi atazugumza na waandishi wa habari hivi punde na matangazo haya yatakuja kwenu moja kwa moja kutoka studio. Baraza la amani na ulinzi la umoja wa Afrika litakutana jijini Abuja nchini Nigeria hii jioni. Miongoni mwa hoja kuu zitakazojadiliwa ni pamoja na hali ya kutatanisha barani humo. Kesho viongozi kumi na tano wa nchi za Afrika watawasili jijini Abuja kuweka sahihi makubaliano ya msimamo wa umoja wa Afrika.**(Presenter's voice fades down as volume is turned down again)**

79. **TINO:** Jibu lako umelipata sasa? Tunaweza kuanza kazi?

80. **BERI:** Ndio. Tuanze kazi!

81. **SFX: CUPS BEING PLACED ON SAUCERS**

82. **MSIMULIZI:** Beri na Tino walifurahia, wakaupa mgahawa kisogo na kuelekea kwenye vituo vyao vipya vya kazi. Ishara za kupiga vita mihadarati zilianza kuonekana. Lakini je, hapa ni mwisho wa hadithi? Tukipumuwa, Jabali alikua akipokea simu za Chambo kutoka kwa watu mbali mbali, vyuo na mashirika. Wengine wakilalama kuwa hakuwatembelea kama walivyopangana na kwamba walihitaji mno huduma yake. Lakini wengine ni wale ambao wanamtafuta baada ya kusifiwa kazi yake na umahiri wake katika vita dhidi ya mihadarati, wakitaka kufanya kazi na yeye, kumfadhili, au hata kumhoji. Mugo, mhariri mkuu wa gazeti la “The Voice”, ni mmoja wao.

**SCENE FOUR: JABALI AT HOME WITH ZULA AND CHAMBO**

83. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

84. **JABALI:** **(tired)** Naapa, hii simu ikilia tena naitumbukiza chooni. **(answers phone with tired, bored voice)** ndio … Haloooo…

85. **MUGO:** Nazungumza na Chambo? Chambo wa shirika la Youth Watch?

86. **JABALI:** **(still bored)** La!!!!!!!!…

87. **MUGO:** Samahani. Labda nimepiga nambari makosa.

88. **JABALI:** Hujakosea nambari. Hii ni simu yake, lakini Chambo hapatikani leo. Tuna fanya kazi na yeye... naweza kukusaidia?

89. **MUGO:** Mfahamishe Chambo kuwa Mugo kutoka gazeti la “The Voice” anataka kumhoji? Tunataka kuangazia kazi zake na jinsi anavyowasaidia vijana walioathiriwa na mihadarati na vileo vyengine, kuishi maisha bora.

90. **JABALI:** Sawa, lakini akirudi tena alivyo.

91. **MUGO:** Unamaanisha nini? Kwani ameondoka?

92. **JABALI:** **(resigned)** Ndio. Tuseme kuwa ameondoka kidogo.

**OUTRO:**

Jabali akisema hayo, tunakamilisha sehemu ya tisa, kwenye kipindi hiki kiitwacho **"Poromoko la jamii".** Kinachoangazia mihdarati na vileo**.** Jiunge nasi kwenye kipindi kijacho na cha mwisho ili ujue hadithi itaisha vipi. Je Chambo atarudi kazini? Au atarudia zaidi madawa ya kulevya? Ukipenda kusikiliza kipindi hiki au vile vilivyotangulia, na hata kutoa maoni yako, basi tembelea tovuti yetu www.dw.de/lbe. Hadi tutakapo kutana tena, kwaheri.